

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG.**

**Simu: (+255) 755350797
686937744**

Email: laghanga@hanangdc.go.tz

**SHULE YA SEKONDARI LAGHANGA
S. L. P 225, KATESH
HANANG –MANYARA
11/12/2020**

KUMB. NA LSS/J.INS/VOL. 1

.....
.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA
SEKONDARI LAGHANGA MWAKA -2021.**

Ninayo furaha kukutaarifu na kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka wa masomo 2021. Hivyo unatakiwa kuripoti shuleni siku ya jumatatu tarehe 11/01/2021 saa 1:30 asubuhi.

Tafadhali fika shuleni ukiwa tayari kupokea, kutekeleza, na kutii maagizo na sheria zote za shule bila usumbufu wowote. Ni matumaini yangu kuwa utatumia nafasi hii vizuri kwa kujifunza kwa bidii ndani na nje ya shule.

Mwanafunzi atakayechelewa ndani ya siku saba (7) tangu siku ya kuripoti, atahesabiwa kuwa hataki nafasi aliyopewa, hivyo nafasi hiyo atapewa mwanafunzi mwingine na **MZAZI/MLEZI ATAKAYEACHA KUMLETA MTOTO WAKE SHULENI KWA KISINGIZIO CHOCHOTE KILE ATACHUKULIWA HATUA KALI ZA KISHERIA.**

MAHITAJI KWA MWANAFUNZI

1. VIFAA VYA DARASANI

- A) Madaftari makubwa 12 (COUNTER BOOK QUIRE 2)
- B) Kalamu (bluu/nyeusi), penseli, rula na mathematical set.
- C) Kamusi ya kiingereza -Oxford

2. CHAKULA

- A) Mahindi **Kg 80**, maharage **Kg 35** na **Tsh 95,000/=**kwa mwaka.(Unaweza kulipa nusu ya mahitaji kwa muhula)
- B) Sahani moja na bakuli moja za kawaida pamoja na kijiko kimoja.

NB: Kwa wanafunzi watakao hitaji kukaa hostel (wavulana na wasichana), wazazi wao wafanye mawasiliano na uongozi wa shule mapema kuomba nafasi hiyo.

Aidha, mahitaji ya hostel ni kama ifuatavyo;

- i. Mahindi **Kg 160**, maharage **Kg 70** na **Tsh: 190,000/=**kwa mwaka, ambapo unaweza kulipa nusu kwa muhula.

- ii. Ndoo ndogo mbili, sahani au bakuli mbili, kikombe, na kijiko (spoon).
- iii. Vifaa vya usafi wa mazingira ambavyo ni jembe na fagio
- iv. Godoro ndogo za futi mbili na nusu kwa sita
- v. Sare za hosteli ni sketi rangi ya kaki, tisheti au flana ya bluu, traksuti nyeusi au bluu, mashuka rangi ya bluu au pink, blanket na chandarua. **malipo yote ya fedha yalipwe kupitia akaunti ifuatazo: 41010006375, NMB (Kamati ya Chakula Laghanga Sekondari)**

3: SARE ZA SHULE

- A) Suruali mbili (2) kwa wavulana, mkanda mweusi wa ngozi na Rangi ya kitambaa ni kijani (jani la mgomba).
- B) Sketi mbili (2) kwa wasichana rangi ya kijani (jani la mgomba).
- C) Shati za rangi nyeupe mbili (2) mikono mifupi
- D) Sweta za rangi ya kijani mbili (2)
- E) Soksi kwa wasichana rangi nyeupe (stocking) pea mbili (2) na wavulana soksi za khaki pea mbili (2)
- F) Nguo za michezo-fulana mbili (2) za bluu zisizokuwa na maandishi na bukta mbili (2) za bluu.
- G) Viatu vyeusi kwa wavulana na wasichana vyenye kamba **NA VISIVYO VYA KISIGINO KIREFU, PLASTIKI (BAJAJI) AU BUTI .**

MUHIMU: NI MARUFUKU KUVAA NGUO FUPI NA MLEGEZO KWANI KUFANYA HIVYO NI KUKIUKA MAADILI KWA MAKUSUDI, NA UKIBAINIKA HATUA KALI ZITACHUKULIWA DHIDI YAKO.

KARIBU SANA SUMAYE SEKONDARI

SINKAMBA CM.
MKUU WA SHULE